# Wahojiwa kuhusu vifo vya watu kula samaki anayedaiwa kuwa na sumu

Na Julieth Mkireri, MAFIA

WATU watatu wanashikiliwa na Jeshi la Polisi Wilaya ya Mafia kwa mahojiano kutokana na vifo vya watu saba vinavyosadikiwa kutokea baada ya kula nyama ya samaki aina ya kasa anayedaiwa kuwa na sumu.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi wa Rufiji, Canute Msacky, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Machi 12, mwaka huu, majira ya saa 1:00 usiku katika kaya nne tofauti wilayani Mafia.

Katika taarifa yake, Kaimu Kamanda huyo alisema watuhumiwa hao nao ni kati ya waliokula samaki huyo na wamelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mafia wakipatiwa matibabu huku wakiwa chini ya ulinzi.

Aliwataja waliofariki dunia baada ya kula samaki huyo kuwa ni Abdallah Nyikombo (4), Makame Nyikombo (9), Ramadhani Karimu (miezi minane), Minza Hatibu (miezi 10), Salima Mjohi (28), Mohamed Makame (miezi saba) wote wakazi wa kijiji cha Bweni na Ally Selemani (miezi minane) mkazi wa kijiji cha Kanga.

Kamanda Msacky alisema miili ya marehemu imefanyiwa uchunguzi wa kitabibu katika hospitali ya wilaya ya Mafia na kukabidhiwa kwa ndugu kwa taratibu za mazishi na kwamba chanzo cha tukio kinaendelea kuchunguzwa.

Msacky alitoa wito kwa wavuvi kuacha tabia ya kuvua samaki aina ya kasa kwa kuwa ni nyara za serikali na kwamba wanatakiwa kufuata taratibu na sheria za uvuvi wa samaki hao.

Alisisitiza kuwa Jeshi la Polisi linaendelea kuchukua hatua kali kwa wavuvi wasiofuata taratibu na sheria za nchi.

# Rais Dk. Samia atoa bilioni 266.7/- ujenzi bandari ya uvuvi

**Na MWANDISHI WETU**

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Riziki Shemdoe, amemshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa jumla ya sh. bilioni 266.7 kugharamia ujenzi wa mradi wa bandari ya uvuvi Kilwa Masoko, mkoani Lindi.

Profesa Shemdoe alisema hayo juzi Kilwa, mkoani Lindi alipotembelea bandari hiyo akiwa katika ziara ya kikazi.

"Ninamshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuridhia sh. bilioni 266.7 kugharamia mradi wa ujenzi wa bandari ya uvuvi hapa Kilwa Masoko mkoani Lindi," alisema.

Alisema bandari hiyo ikikamilika itakuwa msaada mkubwa kwa Watanzania wanaojishughulisha na uvuvi, kwani itazalisha ajira 30,000 kwa vijana wa kike na kiume, ikiwemo kuongeza usafirishaji wa samaki nje ya nchi na tija ya uvuvi katika bahari kuu.

Katibu huyo aliainisha faida nyingine bandari itapunguza upotevu wa samaki, itaondoa changamoto ya uvuvi haramu na kutolewa taarifa.

Pia, itapunguza changamoto ya upungufu wa samaki ndani ya nchi, ikiwemo kuongeza mchango wa sekta ya uvuvi kutoka asilimia 1.71 mwaka 2023 hadi asilimia 3-5 ifikapo mwaka 2026.

Profesa Shemdoe alisema tayari Rais Samia ameridhia malipo ya awali ya sh. bilioni 40 zilizolipwa kwa mkandarasi anayejenga bandari hiyo.

Aidha, katibu huyo alikutana na mkandarasi anayejenga bandari hiyo kampuni ya China Harbour Engineering Company Ltd na mshauri elekezi Kampuni ya Dar Al-Handasah Consultants na kuwaelekeza wafanye kazi kwa bidii wamalize ujenzi katika muda uliopangwa.

Kwa upande wake, mkandarasi anayejenga bandari hiyo na mshauri elekezi walikubali kufanya kazi usiku na mchana kuhakikisha mradi huo unakamilika katika muda uliopangwa.

# Milk prices up by 25pct over low supply in Tanga

By Correspondent Cheji Bakari, Tanga

MILK prices have risen by between 25 and 30 percent over the last two months in Tanga Region; a good news to farmers but bad news for consumers.

The increased prices is being caused by decreased supply of milk as climate change, specifically ongoing dry season and high temperature, have dried pastures and water sources, which have stressed cattle health conditions.

Livestock keepers who mostly depend on livestock as their main source of livelihood, also say the situation has affected their income, as the quantities of milk they are currently producing are lower than during the last quarter of 2022.

The survey by the Guardian has shown that one litre of cattle milk is currently sold at between 1,200/- to 1,300/- from 1,000/- recorded between December 2022 and January 2023.

The survey carried out for number of days this month in Muheza, Tanga, Mkinga and Pangani districts, which are the main sources of milk, has found that the increased market stress is due to rising in demands, and low production.

Speaking with the Guardian last week, some of the livestock keepers outlined various reasons causing undersupply of milk, the major one being the dried up of pastures, legumes and water channels they used to graze their cattle herds.

"The rising temperature is reducing animals' health, led to additional loss of milk production as well as reproduction," said Lukumay Akyoo Duga, the Mafironi village's livestock keeper in Mkinga district.



"Even milk retailers from Lunga Lunga in Kenya are currently crossing to Horohoro border post, ordering milk from Tanzanian side, because their main milk producers have also been affected by the same climatic condition."

Father Roberto Jacues Italian missionary who owns dairy cattle ranch in Muheza district, stated that heat stress is one of the greatest challenges they are facing as producers, causing the decreasing milk production, hence pushing up consumer prices.

"Warm climates depress feed intake, milk production, and reproductive performance of our cows. I am now spending a lot of money to hire local people to find and buy forage and water from distance, a situation that increased the cost of feeding my cattle; which has therefore forced me to increase the price of milk," stated Father Roberto who is also a major supplier of milk to Muheza, Korogwe and Dar es Salaam.

However, when reached for comments through his phone, the Tanga Dairy Cooperative Union (TDCU) chairman Hamis Mzee was not reachable.

One of the leaders, who preferred to remain anonymity on condition that he is bounded by the union's mandate not to speak, stated that the situation has also decreased dairy products at Tanga Fresh Milk processing factory.

Young women tech

# Sita wafa kwa kula kasa, watatu walazwa

Baraka Loshilaa, Mwananchi
bloshilaa@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Watu sita wa familia tofauti wilayani Mafia mkoani Pwani wamepoteza maisha na wengine watatu kulazwa hospitalini baada ya kula samaki aina ya kasa, Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Kipolisi Rufiji, Kanuti Msaki amethibitisha.

Akizungumza jana kwa njia ya simu, Kamishna Msaki alisema tyote hayo yalijiri Machi 12 jioni baada ya wavuvi kumpata kasa huyo na kugawana nyama yake kwa matumizi ya familia.

"Inavyoonyesha wazazi ndio walikuwa wavuvi sasa walipompata kasa wakagawana na kupeleka kitoweo nyumbani. Waliopoteza maisha jumla yao wapo sita," alisema Kamanda Msaki.

Kamanda alisema kati ya waliopoteza maisha ni mtoto wa miezi 10 huku wanaume watatu wakilazwa hospitalini.

Msaki aliwaonya wavuvi kuepuka kuvua skasa ambao Serikali ilishapiga marufuku uvuvi wake.

"Wananchi wanaoitumia bahari kwa uvuvi watambue kuwa samaki aina ya kasa haruhusiwi kuvuliwa," alisisitiza kamanda huyo.

Mwajuma Abdallah, mkazi wa Kijiji cha Bweni wilayani humo akiwa Kituo cha Afya Kirongwe na wajukuu zake wakitibiwa baada ya kula nyama ya samaki huyo aliiambia *Mwananchi* kwa njia ya simu kwamba walikumbwa na kadhia hiyo baada ya kula samaki waliyepewa na jirani yao.

"Mimi sikuwepo nyumbani nilikuja jana (juzi), mkwe wangu na mtoto wake baada ya kula nyama ya samaki huyo walipoteza maisha, hapa hospitalini nipo na watoto wake wawili wanapatiwa matibabu Kituo cha Afya Kirongwe," alisema.

**Kasa ana sumu.....**

Alipozungumza na *Mwananchi* mwaka juzi, Mkurugenzi wa Uvuvi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Emmanuel Bulayi alisema wapo kasa wenye sumu na wasio na sumu.

"Kama ilivyo kwa nyoka, wapo wenye sumu na wasio na sumu basi hata kasa iko hivyo. Sumu hii inaweza kutokana na walivyoumbwa au hata miili yao kuwa na uwezo wa kuhifadhi sumu inayotengenezwa kutokana na vimelea wanavyokula," alisema Bulayi.

Daktari Mkuu wa Hospitali ya Kivunge iliyopo Mkoa wa Kaskazini Unguja, Tamim Said alisema samaki huyo ana sumu ambayo kwake haina madhara ila inamdhuru binadamu.

"Ile sumu kwa kasa mwenyewe inakuwa si tatizo lakini kwa binadamu ni shida kubwa na inategemea kiwango cha nyama kilicholiwa kina sumu kiasi gani, na sumu hii huwaathiri zaidi watoto kwa sababu uwezo wao wa kinga mwili kuhimili unakuwa bado mdogo," alisema Dk Said.



**10**
Umri wa miezi ya mtoto mdogo zaidi aliyefariki kwa kumla kasa mwenye sumu wilayani Rufiji.

> "Wananchi wanaoitumia bahari kwa uvuvi watambue kuwa samaki aina ya kasa haruhusiwi kuvuliwa.'
>
> Kanuti Msaki, kamanda wa Polisi Rufiji.

**Mjue kasa**

Wataalamu wanasema kuna aina kuu nane za kasa duniani ambao ni Green Turtle (kasa wa kijani au kawaida), Hawksbill Turtle (ng'amba) loggerhead Turtle (kasa duvi), Atlantic Ridley, Pacific Ridley, Scute covered shell Turtle, Leatherback (kasa ngozi) na Olive Ride (kasa muanzi).

Licha ya kasa kufanana sana na kobe, yeye hawezi kurudisha kichwa chake ndani ya gamba kwa kuwa ni kilaini na miguu ya wavuti inayomsaidia kuogelea kwa kasi majini.

Kasa anao uwezo wa kubana pumzi kwa takriban saa tano akiwa majini. Chakula kikubwa cha viumbe hawa ni mimea ya baharini kama vile yavuyavu, mwani, kaa, kamba na matumbawe.

Kasa ni viumbe wa baharini anayetajwa kuwa na kumbukumbu kubwa katika kundi la reptilia.

Kasa jike anao uwezo wa kurudi katika fukwe za bahari ileile aliyototolewa, licha ya kuwa huwa na tabia ya kusafiri kutoka bahari moja hadi nyingine ila muda wa kuzaliana unapofika, hurudi kwenye ufukwe aliotokea awali kusudi atage mayai na kuyaangua.

Kama ilivyo kwa reptilia wengi, kasa hawezi kuatamia mayai yake bali huchimba kiota na kuyafukia mpaka yatakapototolewa.

Wenje alia ugumu wa maisha, Lema awakomalia bodaboda

MIAKA MIWILI YA RAIS DK.SAMIA

# CCM Zanzibar yajivunia mafanikio uchumi buluu

NA WILLIAM SHECHAMBO

WAKATI Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akiarajiwa kutimiza miaka miwili madarakani, Machi 19, mwaka huu, Zanzibar inaendelea kujivua mafanikio ya kiuchumi yanayochagizwa na utekelezaji wa dhana ya uchumi wa buluu.

Kimsingi katika miaka ya hivi karibuni, ukitamka msamiati uchumi wa buluu, kwa sasa si neno jipya tena, hususan katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Uchumi wa buluu 'Blue Economy' ni aina ya uchumi unaotegemewa zaidi duniani katika kuongeza pato la Taifa kupitia rasilimali za bahari.

Hii inajumuisha shughuli zote zinazohusisha eneo la bahari na faida zinazotokana na matumizi sahihi ya rasilimali hiyo, katika kuinua uchumi kwa lengo la kuimarisha maendeleo ya mtu na taifa kwa ujumla.

Mataifa mbalimbali duniani, yamekuwa mstari wa mbele kusimamia na kuendeleza uchumi wa buluu, ambao kwa Tanzani Visiwani tayari umethibitishwa kuung'arisha uchumi wa Zanzibar.

Katibu wa Halmashauri Kuu (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi, Zanzibar, Khamis Mbeto Khamis, amekuwa mmoja kati ya watu waliokiri kuwa uchumi wa Zanzibar unaendelea kuimarika kupitia dhana hiyo ya uchumi.

Anasema ni wazi kuwa Zanzibar ni nchi ya visiwa, ambapo wananchi wake wanategemea kilimo na uvuvi katika kuendesha maisha yao ya kila siku.

Khamis anasema, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar(SMZ), awamu ya nane, inayoongozwa na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi wa CCM, imetambua umuhimu wa rasilimali bahari na kuwekeza nguvu kubwa kila uchao.

Mwenezi huyo wa Zanzibar, ambaye alikuwa na ziara ya siku moja ya kutembelea vyombo vya habari wa Chama, ikiwemo Uhuru Publication Ltd, anawaeleza wanahabari wa Uhuru kwamba Rais Samia kwa kushirikiana na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, wamekiongoza Chama kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020-2025.

Ilani ya uchaguzi imezungumza kinagaubaga juu ya dhana ya uchumi na buluu na mpango wake wa kumsaidia mwananchi kiuchumi.

"Zanzibar ya sasa ni suala lingine kabisa, tunafanya makubwa kupitia dhana ya uchumi wa buluu, tunajenga bandari kubwa, tumewekeza katika uvuvi kwa kushirikiana na benki mojawapo kwa kuwakopesha wavuvi wadogo boti za kisasa za uvuvi," anasema.

Khamis anasema, mkopo huo wenye thamani ya sh. bilioni 16.5, unahusisha utoaji wa boti zenye teknolojia ya kisasa ya utafutaji samaki na mfumo wa kusoma jiografia 'rada' ili kuwarahisishia kazi wavuvi 280 kutoka Unguja na Pemba.

Pamoja na hatua hiyo, anasema kumekuwa na mazungumzo na pande mbalimbali katika uwekezaji wa miundombinu baharini, ikiwemo michezo ya majini 'aquatic sports' na ujenzi wa hoteli za nyota tano



RAIS wa Zanzibar Dk.Hussein Ali Mwinyi, akiwa katika mazungumzo na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, mazungumzo yaliofanyika katika ukumbi wa Ikulu Jijini Zanzibar.

"
**Zanzibar ya sasa ni suala lingine kabisa, tunafanya makubwa kupitia dhana ya uchumi wa buluu, tunajenga bandari kubwa, tumewekeza katika uvuvi kwa kushirikiana na benki mojawapo kwa kuwakopesha wavuvi wadogo boti za kisasa za uvuvi... Khamis Mbeto Khamis, Katibu wa Halmashauri Kuu (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi, Zanzibar,**



KATIBU wa NEC, Idara ya Itikadi na Uenezi CCM Zanzibar, Khamis Mbeto Khamis.

ambazo ni sehemu tu ya miradi 215 itakayotekelezwa maeneo mbalimbali.

Anasema miradi hiyo ina thamani ya dola za Marekani bilioni 300.29 sawa na zaidi ya sh. trilioni 2, ambapo itatekelezwa katika visiwa 16 vinavyopatikana pembezoni mwa Pemba na Unguja.

Kwa upande wa Tanzania Bara, anasema uchumi unapaa kwa kuwa hakuna eneo ambalo unaweza kupita, bila kukuta mradi mkubwa wa maendeleo ambao Rais Dk. Samia ameweka fedha za utekelezaji wake.

Anasema, miradi hiyo ya kimkakati itawasaidia kwa kipindi cha muda mfupi na mrefu wananchi kujikimu kimaisha, kwa kuwa msingi wa utekelezaji wake ni kuwagusa wananchi wa maeneo husika.

"Hakuna mkoa utakaopita hapa Tanzania, ukakosa mradi wa Mama Dk. Samia, hakuna kote ameweka fedha, kote," anasema.

UJENZI WA BANDARI

Khamis anafafanua kuwa, ujenzi wa bandari ya mafuta ya Mangapwani, utakuwa na mchango mkubwa wa kuitambulisha Zanzibar na Tanzania kwa ujumla duniani kupitia sekta ya uchukuzi wa mafuta baharini hivyo kuinua uchumi.

Anasema bandari hiyo itakayokuwa na bohari ya kuhifadhi mafuta, itakuwa na uwezo wa kuhifadhi mafuta lita za ujazo milioni 25 kwa mwezi, hali itakayofungua masoko ya kimataifa.

KILIMO CHA UMWAGILIAJI

Mwenezi huyo anasema, pia Zanzibar wakati ikifurahia miaka miwili ya Rais Dk. Samia madarakani, inatekeleza miradi ya skimu za umwagiliaji yenye thamani ya sh. bilioni 25, kuwasaidia wakulima kulima zaidi ya mara tatu kwa mwaka.

"Lengo letu ni kuwafanya wakulima walime kwa zaidi ya mara mbili au mara tatu kwa mwaka, wasiathiriwe kabisa na mabadiliko ya tabia nchi, hii itafanya wananchi wengi zaidi wajikite katika kilimo," anasema.

Vilevile, anasema kupitia ujenzi wa Kiwanja cha kisasa cha ndege Pemba, Zanzibar inatarajia ujio wa ndege kubwa katika kisiwa cha Pemba hivyo kufungua fursa za utalii wa baharini kwa wakazi wa kisiwa hicho.

Anasema, ujenzi wa kiwanja hicho unaambatana na ujenzi wa barabara kubwa zenye